BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya Chukuwani, Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,
Zanzibar, Tanzania

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA USTAWI WA JAMII KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,**

Awali ya yote napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, mwingi wa rehema, aliyetujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana leo hii ndani ya Baraza letu kuendelea na majukumu yetu ya Kitaifa. Namuomba Mola wetu anijaalie ufasaha katika uwasilishaji wa Hotuba hii na atupe usikivu na uelewa ili tuweze kuichangia kwa umakini wa hali ya juu na hatimae kuipitisha bajeti hii iliopo mbele yetu kwa maslahi ya Taifa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inatoa pongeza za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, pamoja na wasaidizi wake Makamu wa Kwanza wa Rais Mheshimiwa Othman Masoud Othman na Makamu wa Pili wa Rais Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla kwa kumsaidia vyema Mheshimiwa Rais katika kutekeleza majukumu yake ya kuiongoza nchi

hii, sambamba na jitihada anazozichukua za kuendeleza sekta ya michezo nchini.

**Mheshimiwa Spika,**

Aidha, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Baraza kwa namna mnavyoliendesha Baraza kwa umahiri mkubwa, namuomba Mwenyezi Mungu awazidishie busara na hekima katika kutekeleza jukumu la kutuongoza ili tuweze kutekeleza vyema wajibu wetu katika chombo hiki muhimu kwa nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Pia napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri,Katibu Mkuu,Wakurugenzi na Watendaji wote wa Wizara ya Habari,Vijana ,Utamaduni na Michezo kwa kuweza kusimamia vyema Mradi wa Ukarabati wa Uwanja wa Amani Unguja na Kiwanja cha Gombani Pemba kwa mafanikio makubwa na kuboresha miundo mbinu ya kisasa ili viweze kutumika katika mashindano ya kitaifa na kimataifa .

**Mheshimiwa Spika,**

Pia tunapenda kuipongeza Wizara ya Habari,Vijana Utamaduni na Michezo kwa mashirikiano waliyotupatia Kamati wakati wa kupitia Makadirio ya Bajeti ya Mwaka 2024/2025 ya Wizara hii.

Pia nichukue nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati yetu kwa umoja wao na kazi nzuri waliyoifanya kiasi cha kunirahisisishia kazi ya kuongoza kikao kuwa nyepesi na ya ufanisi. Kwa kweli, ni wajumbe Mahiri, ambao wameweza kuyajadili kwa kina na ipasavyo makadirio hayo na kuhoji mambo mbali mbali kwa lengo la kuhakikisha kwamba

fedha wanazoidhinisha zinatumiwa kwa matumizi yaliokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa heshima napenda kuwatambua Wajumbe hao kwa majina kama hivi ifuatavyo: -

| | | | |
|---|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Sabiha Filfil Thani | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Nassor Salim Ali (Jazira) | Makamu Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Abdulla Hussein Kombo | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Haji Omar Kheri | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Salma Mussa Bilal | Mjumbe |
| *7.* | Mhe. Bahati Khamis Kombo | Mjumbe |
| *8.* | Mhe. Sulubu Kidongo Amour | Mjumbe |

Aidha, Kamati yetu inafanyakazi na makatibu Watatu (3) ambao kwa kiasi kikubwa wamekuwa wakitusaidia sana katika kutekeleza majukumu yetu, Makatibu hao ni:

| | | |
|---|---|---|
| 1) | Ndg. Salha Abdulla Abdulla | Katibu |
| 2) | Ndg. Talib Enzi Talib | Katibu |
| 3) | Ndg. Bakari Makame Haji | Katibu. |

**Mheshimiwa Spika,**

Moja kati ya jukumu la msingi la Kamati yetu ni kuchambua mapendekezo ya Serikali, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya kila mwaka, hivyo katika kutekeleza jukumu hilo Kamati yangu

ilikaa na kuijadili na hatimaye kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari Vijana, Utamaduni na Michezo, sasa kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Kamati, napenda kuwasilisha Maoni ya Kamati kuhusiana na Bajeti hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inapongeza utekelezaji wa Bajeti ya Wizara katika mwaka wa fedha 2023/2024. Hata hivyo Kamati inaishauri kufanyiwa kazi changamoto zilizojitokeza katika baadhi ya Taasisi kama tulivyoeleza katika Ripoti Kuu ya Kamati ya Mwaka 2023/2024. Baadhi ya Changamoto hizo ni kama;

**Shirika la Utangazaji ZBC**

- Kamati inaishauri Wizara kuharakisha kukamilisha uwepo wa Sheria mpya ya ZBC Namb.4 ya mwaka 2013 ambayo ni ya muda mrefu sambamba na ufanywaji wa mapitio ya kuwa na Kanuni ya Sheria hiyo.

- Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Tume ya utumishi Serikalini kukamilisha kwa hatua zilizobaki marekebisho ya Mapendekezo ya Muundo mpya wa Shirika ili kuweza kutambua baadhi ya nafasi ambazo katika sheria hazikuwemo.

**Idara ya Sanaa**

- Kuwepo kwa uhaba wa fedha katika Idara ya Sanaa na kusababisha kushindwa kutekeleza majukumu ya Idara kwa mwaka 2023/2024. Kamati inaishauri kupatiwa fedha Idara hii ili kazi za Sanaa ziweze kutekelezwa kwa ufanisi.

*Ukarabati na uboreshaji wa uwanja wa Amani na Gombani Pemba*

- Kamati inaishauri Wizara ya fedha kuhakikisha inakamilisha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kukamilisha kazi za miradi iliyobaki pamoja na Wizara husika kuhakikisha inasimamia vyema awamu iliyobaki ili kazi ya uimarishaji wa viwanja vya michezo vya Amani Complex na Gombani iweze kukamilika.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ina mafungu mawili (2) ambayo ni **J03** (Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo). Fungu hili limepanga kutekeleza Program Kuu Nne (4) na Program Ndogo nane (8) ambazo zinakadiriwa kutumia jumla ya Shilingi Bilioni **89,291,932,000/=** Makadirio ya Mapato katika Fungu hili ni Shilingi Milioni **575,000,000/=**

**Fungu J05** (Tume ya Utangazaji) limepanga kutekeleza Programu Kuu Mbili (2) na Program Ndogo Tatu (3) ambazo zinakadiriwa kutumia jumla ya shilingi Bilioni **1,484,200,000.**

**FUNGU J03**

**PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA HABARI, UTANGAZAJI NA UCHAPAJI**

**Mheshimiwa Spika,**

Programu Kuu hii inatekelezwa chini ya Programu Ndogo mbili (2) ambazo ni SJ030101 Upatikanaji na Usambazaji wa Habari na SJ030102 Usimamizi wa Vyombo vya Habari, Utangazaji na Uchapaji, ambapo inatarajia kutekeleza vipaumbele kama;

- kutoa huduma za uchapishaji kwa taasisi za Serikali na Binafsi,
- kutoa huduma za Bohari kuu ya vifaa vya ofisi na kuandikia kwa Taasisi za Serikali na Binafsi
- kuendeleza biashara ya Ving'amuzi pamoja na Maudhui yenye kuelimisha na kuburudisha
- kuendeleza na kusimamia Gazeti la Serikali
- na kudhibiti na kusimamia shughuli za utangazaji kupitia Sera na Sheria za Habari na Utangazaji.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Serikali kufanya jitihada za kulipatia Shirika la Magazeti mtambo wake wa uchapishaji wa magazeti ili kuepuka gharama kubwa za uchapishaji kwa kampuni binafsi na kuliwezesha Shirika kufanya kazi zake kwa ufanisi.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA VIJANA

**Mheshimiwa Spika,**

Programu hii ya PJ0302 ina program ndogo moja (1) ambayo ni ya Maendeleo ya vijana (SJ030201), na inakadiriwa kutumia shilingi Bilioni **5,662,714,000/=** kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaipongeza Wizara kwa kujenga hoja serikalini na kuweza kupatiwa Fungu kwa ajili ya Mradi wa Vijana ambapo katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara haikupangiwa makadirio ya fedha katika Mradi huo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inashauri Miradi ya Vijana kuwa endelevu kwa kutengewa fedha za kutosha ili Vituo vya kuwaendeleza vijana viwe na miundombu ya

kisasa itakayoweza kuwasaidia vijana kujiendeleza katika sekta mbali mbali na kuingia kwenye soko la ajira au kuweza kujiajiri.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO.

**Mheshimiwa Spika,**

Programu hii ya PJ0303, ina Programu Ndogo mbili (2) ambazo ni SJ030301(Uimarishaji,uhifadhi na Uwendelezaji wa Utamaduni, Sanaa na Ubunifu) na SJ030302 (Uimarishaji wa Michezo na Miundombinu ya viwanja vya michezo. Program Kuu PJ0303 imekadiriwa kutumia Shilingi Bilioni 69,216,860,000 kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya Sanaa,ujenzi wa viwanja vya wilaya ,ujenzi wa viwanja vya michezo Maisara.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inapenda kuchukua fursa hii kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuendelea na maboresho ya viwanja vya michezo vya kisasa na kujenga viwanja vipya vya michezo kwa kila Wilaya za Unguja na Pemba. Sambamba na ujenzi wa nyumba ya Sanaa ambayo itakwenda kusaidia katika kutunza kazi za Sanaa na uendelezaji wa utamaduni nchini.

Aidha, Kamati inaishauri Wizara kabla ya kuanza ujenzi wa viwanja iwashirikishe wataalamu wa fani za michezo kuweza kushauri mambo ya msingi ili kupunguza gharama za ziada zisizokuwa na ulazima na kupunguza mzigo kwa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Wizara kuvitunza viwanja hivyo vya kisasa na

kuangalia uwezekano wa kuingia mikataba na sekta binafsi katika kuvisimamia na kuepusha uharibifu wa miundombinu kwa kuendeleza usafi na ulinzi ili viwanja hivyo vionekane katika taswira nzuri na ya kuvutia.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaendelea kuipongeza Serikali kwa kupitia Baraza la Sanaa na filamu Zanzibar (BASFU) kwa kuweza kuzifungia nyimbo na filamu zote zisiso na maadili ambazo zinaenda kinyume na silka na utamaduni wa Mzanzibar.

**PROGRAMU KUU YA UTAWALA NA UENDESHAJI**

Programu ya PJ0304 ina Programu Ndogo tatu (3) ambazo ni SJ030401(Mipango sera na utafiti), SJ030402(Utumishi na uwendeshaji) na SJ030403(Uratibu wa shughuli za wizara Afisi Kuu Pemba). Katika fungu hili imekadiriwa kutumia shilingi Bilioni 4,017,802,000/= kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025 ambapo baadhi ya vipaumbele vilivyopangwa kutekelezwa ni kama vifuatavyo;

- kuratibu na kusimamia Mipango, Sera na Tafiti za Wizara
- kuratibu, kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa Programu za Miradi na shughuli za Wizara
- na kujenga uwezo na mazingira mazuri ya kazi kwa wafanyakazi.

**FUNGU J05 TUME YA UTANGAZAJI.**

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaunga mkono uamuzi wa Serikali wa kuipatia Wizara Fungu jipya la **J05** lenye **Programu Kuu ya Maendeleo ya Habari na Utangazaji (PJO501)** na **Programu Kuu ya Utumishi na Uwendeshaji(PJ0502)** lenye

jumla ya Makadirio ya fedha ya shilingi **Bilioni 1,484,200,000**.

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati inaipongeza Serikali katika Bajeti ya mwaka 2024/2025 kwa kuweza kuipatia Tume ya Utangazaji fedha zitakazokusanywa (retantion) zibaki ili ziendeleze kazi katika Taasisi hiyo. Kamati inaishauri Tume ya Utangazaji kuhakikisha kuwa fedha zitakazokusanywa zinatumika vizuri na zinaleta ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,**
Mwisho, napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa utulivu wa hali ya juu wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha Hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika,**
Aidha, kwa vile Kamati imepitia, imejadili na kuyakubali mapendekezo Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Sasa niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu waijadili, watoe ushauri pamoja na mapendekezo yao na hatimae waiunge mkono Bajeti hii ili wamuwezeshe Mheshimiwa Waziri kufanikisha na kutekeleza yale waliojipangia katika mwaka wa fedha ujao.

**Mheshimiwa Spika,**
Baada ya kusema hayo naunga mkono hoja.

**Mheshimiwa Spika,**
Naomba kuwasilisha.

……………………………………

Mhe. Sabiha Filfil Thani,

Mwenyekiti,

Kamati ya Ustawi wa Jamii,

**BARAZA LA WAWAKILISHI,**

**ZANZIBAR.**